# KWA NINI KUIAMINI BIBLIA

## Mungu Anaangalia Neno Lake

iliyoandaliwa na
Walter Eric

06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 1 27-05-2022 14:25:45

Kichwa cha asili cha kitabu: Let the Bible Speak for Itself

© 2022, kwa Toleo la Kiswahili
Life Challenge
P.O. Box 50770-00200,
Nairobi, KENYA
**www.life-challenge.org**

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya kitabu hiki inayoruhusiwa kunakiliwa bila idhini ya maandishi, isipokuwa kwa nukuu fupi katika vitabu na mapitio.

Nukuu zote za Kurani zimetolewa kwenye: KURANI TAKATIFU, iliyofasiriwa na Sheikh Abdullah Saleh Farsi, chapa ya saba, 1993.

Nukuu za Biblia zimetolewa kwenye: NENO BIBLIA TAKATIFU, 2014.

Kimetafsiriwa na John Augustine Mabutagulwa, Zanzibar, Tanzania.

ISBN: 978-9966-895-90-5

Kimechapishwa nchini Kenya.

06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 2 27-05-2022 14:25:45

# Kwa nini kuiamini Biblia

## DIBAJI

Machapisho mengi ya Kiislamu yamefurika kwenye soko miaka ya hivi karibuni. Kwenye mwambao wa pwani ya Afrika ya Mashariki, Sheikh Ali Muhsin, mzaliwa wa Zanzibar, aliyeandika pia shairi lenye aya 1300 kuhusu maisha ya Mtume, ameandika "Acha Biblia Izungumze", kijitabu kilichochapishwa kwa wingi. Ujumbe wake umeenea kwa njia ya kanda kutoka misikitini, magari ya abiria, na majumbani kwenye pwani yote ya Kenya. Machapisho mengine kama "Uislamu kwenye Biblia", "Yesu, Mtume wa Uislamu" na "Injili ya Barnaba" iliyoenea sana, hayo nayo huhamasisha mwitikio wa Kikristo. Kijitabu hiki hakikusudii kulenga kila hoja kwenye machapisho yale, bali hasa kutoa sababu za Wakristo kote duniani kuikubali hali ya kuaminika ya Biblia Takatifu.

Tunapenda rafiki zetu Waislamu wafahamu kwa nini Wakristo hawaamini kuwa Biblia imepotoshwa. Huu si uamuzi wa kimhemko, bali hasa hutokana na hoja zenye maana baada ya kutazama kwa uangalifu ukweli wenyewe. Utakuwa ujinga kudhani kuwa ye yote anaweza kufahamu kikamilifu kila kipengele cha ufunuo wa kimungu tuliopewa kwenye maandiko ya Agano la Kale na Agano Jipya, hata hivyo tunaamini kuwa kutofahamu kila jambo kunatokana na upungufu wa akili ya mwanadamu, na si dosari kwenye vitabu vilivyofunuliwa.

Msomaji mwaminifu atapendezwa na uwasilishi huu ulio wazi wa imani yetu katika kuaminika kwa kitabu chetu, akiusoma ushahidi yeye mwenyewe.



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 1 27-05-2022 14:25:45

# 1. UTANGULIZI KWENYE AGANO LA KALE NA AGANO JIPYA

Inaonekana kama vile ilikuwa jana tu nilipokuwa na rafiki yangu tukitembelea kijiji chenye Waislamu wengi Magharibi mwa Kenya. Mara baada ya mazungumzo ya kirafiki na mzee wa kijiji, vijana kadhaa wa kiume walijiunga kwenye mazungumzo yetu, na mmoja wao akasema, “Mnapaswa kuisoma Injili ya Barnaba”. Nikauliza, “Kwa nini unadhani hivyo?” Akajibu, “Ni kitabu kizuri kwa Wakristo kukisoma”. Nikamwuliza nikitaka kujua, “Ni nini kinachokufanya uamini hivyo? Wewe mwenyewe umekisoma?” Alikuwa hajakisoma. Walimwambia wengine na yeye akaamini na kuamua hivyo. Kwa kuwa nilikijua vema kitabu kile, niliweza kuonyesha maeneo mengi ambamo injili hii batili hupingana na Kurani na ukweli mwingi wa kihistoria na kijiografia. Hali hii ya andiko hilo hulionyesha dhahiri kuwa ni udanganyifu ulioandikwa karne nyingi baada ya matukio yenyewe.

Hili si tukio la kipekee. Kama inavyoweza kutarajiwa, kila wakikutana Wakristo na Waislamu mazungumzo haya lazima yahusu Biblia na Kurani, maandiko yanayoheshimika ya imani hizo mbili zinazohusika. Mimi kama Mkristo hili limenihamasisha sana kuifahamu Kurani na fundisho lake. Ninaamini kuwa Mkristo hawezi kufanya mazungumzo yenye maana na Mwislamu kuhusu mada za kidini asipokuwa na ufahamu wa imani na desturi za Kiislamu.

Wakati huo huo nimeshangaa kuona kuwa Waislamu wengi hutatanishwa sana kuhusu tabia ya Biblia ya Kikristo, hasa kuhusiana na sehemu zake kuu mbili zinazojulikana kama Agano la Kale na Agano Jipya. Mara nyingi nimekabiliwa na maswali kama haya:



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 2 27-05-2022 14:25:45

- "Kwa nini mna Agano la Kale na Agano Jipya? Kulikuwa na tatizo gani kwenye Agano la Kale hata ikabidi badala yake muwe na Agano Jipya?"
- "Sisi Waislamu tunalikubali Agano la Kale ambalo kimsingi linalingana na Kurani yetu, lakini hatulikubali Agano Jipya ambalo nyinyi Wakristo mmelibadilisha."
- "Kwa nini kuna Injili nne kwenye Agano Jipya lenu?"
- "Kwa nini wachungaji wenu walilibadilisha agano la asili wakaleta agano jipya?"

Maswali haya huletwa mara kwa mara kwenye mazungumzo na Waislamu. Kiujumla mtazamo ulioenea ni kuwa, kuwako Agano Jipya huonyesa kuwa Agano la Kale limebadilishwa. Kwa maneno mengine "Agano Jipya ni toleo la Agano la Kale lililopotoshwa". Mara nyingi sana Waislamu wamewahi kuniambia, "Biblia yenu imebadilishwa", na kila ninapoomba uthibitisho jibu limekuwa, "Mna Agano la Kale na Agano Jipya."

Mara nyingi nimevunjwa moyo na kiwango cha kutojua kwenye jamii ya Waislamu kuhusu tabia na muundo wenyewe wa msingi wa Maandiko ya Kikristo. Bila shaka hili lipo pia kwa Wakristo wengi kuhusiana na vitabu vya Kiislamu vyenye mamlaka, yaani hiyo Kurani, na hata zaidi zile Hadithi.

Maswali hayo na misimamo hiyo hufunua mfuatano wa dosari katika mtazamo wa Waislamu kwenye Biblia ya Kikristo. Inavyoonekana kwangu hali hii ya Waislamu kutoyafahamu yaliyomo kwenye Biblia imewafanya waathiriwe na uongo mwingi kuhusu yaliyomo humo. Hakuna ustahili wala faida wala hekima katika kushikilia udanganyifu, haijalishi inaonekana udanganyifu huo ungeweza kuunga mkono kiasi gani kwenye hiyo imani potovu kuwa Biblia imebadilishwa. Lakini kuna ustahili na faida katika kupata ufahamu wa kweli kuhusu asili ya Biblia ya Kikristo, na sina shaka kuwa kila mmoja atafaidika na uwasilishi wa kweli wa mambo kama yale atakayokuta yamewasilishwa kwenye kurasa za kijitabu hiki.



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 3 27-05-2022 14:25:45

## 2. AGANO LA KALE NA AGANO JIPYA NI NINI?

Biblia ya Kikristo ina sehemu mbili zinazojulikana kama Agano la Kale na Agano Jipya. Kwenye Agano la Kale kuna vitabu 39 na kwenye Agano Jipya kuna vitabu 27. Vitabu hivyo 66 ndiyo Biblia ya Kikristo.

Tuanze kwa kulielezea Agano la Kale. Haya ndiyo maandiko ya Wayahudi, na ukienda kwenye chumba cha vitabu vya Wayahudi ukaomba nakala ya Maandiko yao Matakatifu utapewa Agano la Kale. Wayahudi wenyewe hawalitumii jina hili kwa Maandiko yao, ni jina la Kikristo tunalotumia kuyatofautisha Maandiko hayo na Maandiko yaliyofuata ambayo yanajulikana kama Agano Jipya

Agano la Kale ni kitabu kilichokamilika karibu karne nne kabla ya wakati wa Yesu.[1] Huanza na vitabu vitano vya Musa ambavyo ni Mwanzo, Kutoka, Mambo ya Walawi, Hesabu na Kumbukumbu la Torati. Vitabu hivi vina historia yote ya mwanadamu kuanzia mwanzo wa uumbaji, kisha huangalia hasa kwenye historia ya Waisraeli kuanzia wakati wa Ibrahimu hadi wakati wa tukio kuu la Waisraeli kuondoka Misri wakiongozwa na Musa.

Vitabu 12 vinavyofuata vina historia ya taifa la Israeli na kuinuka kwa manabii wake hadi baada ya wakati wa Daudi ambapo ufalme uligawika zikawa falme mbili baada ya kifo cha Sulemani. Hatimaye kuabudu sanamu na kukosa uaminifu kwa Mungu walikofanya Waisraeli kuliwaletea utumwa na kuhamishwa kulikodumu miaka 70 hadi Mungu alipowakusanya na kuwarudisha tena kimiujiza kwenye nchi yao ya Palestina. Hadi hapa kimsingi vitabu vyote ni vya kihistoria.

---

1 Inahitajika kutambua kuwa Agano la Kale ni kitabu kinachoelezea utendaji wa Mungu kwa taifa la Israeli kuanzia wakati wa uumbaji hadi miaka mia nne na hamsini kabla ya Kristo. Hivyo Agano la Kale ni kitabu kilichokamilika karibu miaka mia nne kabla ya kuja kwa Yesu.

Kisha inafuata sehemu kuu ya pili ya Agano la Kale, yaani vitabu vitano vinavyojulikana kama vya hekima au ushairi, kwa sababu vinazingatia fundisho kuhusu kumjua Mungu na imani tambuzi ya kweli kwa Mungu. Ni maandiko kama Kitabu cha Ayubu (Ayoub kwenye Kurani), Zaburi, nyingi zikiandikwa na Daudi, Mithali za Sulemani na taarifa ya utafiti katika Kitabu cha Mhubiri inayomfanya msomaji kuzingatia maisha yake.

Hatimaye kuna vitabu 17 vilivyobaki vinavyojulikana kama vitabu vya manabii. Vina unabii wa manabii wa baadaye wa historia ya Wayahudi kama vile Yona, Danieli na Ezekieli kati ya wengine. Manabii walikuwa na utendaji wa aina mbili: Walinena wakimwakilisha Mungu kwa wanadamu na walilithibitisha hili kwa kuandika matukio yatakayokuja baadaye ambayo ni Mungu pekee aliyeweza kuyajua. Kutimia kwa unabii huu mamia ya miaka baadaye kulithibitisha kuwa Mungu ndiye mwanzilishi wa vitabu hivi. Hivyo Maandiko ya Agano la Kale yalikamilishwa miaka 450 kabla ya ujio wa kwanza wa Kristo kwenye dunia hii.

Kabla ya kuliendea Agano Jipya tuutamke kwa ufupi msimamo wa Kikristo kwenye Agano la Kale. Tunalikubali kuwa ni Neno la Mungu ambalo halikubadilishwa na lililothibitishwa kuanzia  nyakati za manabii linaowazungumzia (Musa, Daudi, nk.). Tofauti na Waislamu wengi sana, Wakristo wa kweli hawaamini kuwa Neno la Mungu linaweza kubadilishwa au kupotoshwa, hivyo tunalikubali Agano la Kale kuwa ni Neno la Mungu la kabla ya nyakati za Kikristo, ambalo halikubadilishwa na lililo thabiti. Katika hili Wakristo hufuata mfano uliotolewa na Kristo mwenyewe aliyenukuu kila mara kutoka kwenye vitabu vya Agano la Kale kwenye mafundisho na maisha yake yeye binafsi.



Hivyo Agano Jipya ni nini? Ni Maandiko ya Kikristo yanayoanzia kwenye wakati wa Yesu Kristo. Tofauti na Waislamu, Wayahudi hawamkubali Yesu kuwa ndiye Masihi



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 5 27-05-2022 14:25:45

# **Vitabu vya Biblia Takatifu:**

## *Agano la Kale*








HISTORIA
(Vitabu 17)

Vitabu vya Kishairi
(Vitabu 5)

Unabii
(Vitabu 17)

## *Agano Jipya*

HISTORIA
(Vitabu 5)

Nyaraka
(Nyaraka 21)

Unabii
(Kitabu1)



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 6 27-05-2022 14:25:45

na wanalikataa Agano Jipya kwa sababu hii pekee. Lakini kwa kuwa Wakristo wanaamini kuwa kweli Yesu alikuwa mwanadamu aliyetumwa na Mungu, wanayatambua pia Maandiko ya wakati wake kuwa ni Neno la kweli la Mungu.

Agano Jipya nalo linaweza kugawanywa katika sehemu kuu tatu. Ya kwanza ni ile yenye ujumbe wa Injili nne zilizoandikwa na Mathayo, Marko, Luka na Yohana. Hueleza kuhusu maisha na mafundisho ya Yesu na matukio yanayozunguka kuzaliwa, kusulubiwa, kufufuka na kupaa kwake mbinguni. Yesu alipokuwa bado anaishi pamoja na wanafunzi wake, aliwapa ahadi maalumu ya kumpokea Roho Mtakatifu wa kuwakumbusha atakayewakumbusha kuhusu mambo yote waliyoyasikia na kuyaona (taz. Yohana 14:26). Kilichozifuata kwa karibu habari za Injili ni Kitabu cha Matendo kinachojitamkia kuwa ni mwenzi wa Injili kama ilivyoandikwa na Luka (ona Matendo 1:1-4). Kitabu hiki cha historia kina mambo yanayohusu kukua kwa Kanisa la mwanzo kwa njia ya mahubiri na utendaji wa wale wanafunzi wa Yesu walioongozana naye kwa ukaribu zaidi ambao hivi punde walijulikana kama mitume.

Sehemu ya pili ina vitabu ishirini na moja vya maandishi ya hawa mitume kwa makanisa mbali mbali. Yana mafundisho ya msingi ya maisha na Imani ya Kikristo. Tena waandishi waliyaandika haya wakishawishika kabisa kuwa wamehimizwa na Roho wa Mungu (2 Petro 1:21).

Kitabu cha mwisho kinaunda sehemu ya mwisho, na ni kitabu cha kinabii kinachojulikana kama Ufunuo. Kina muhtasari wa matukio yatakayofuata wakati wote wa enzi ya Kikristo na enzi ya milele itakayokuja baada ya siku ya hukumu.



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 7 27-05-2022 14:25:45

***Tunaona:***

Kuna tofauti ya wazi kati ya Agano la Kale na Agano Jipya. Agano Jipya lilikusanywa ndani ya miaka 60 ya mwanzo baada ya kufufuka kwa Kristo, na hivyo ilikamilika kama miaka 500 baada ya Agano la Kale. Si upotoshaji, urekebishaji wala ubadilishaji wa Agano la Kale. Ni kitabu tofauti kabisa na kimewekwa sambamba na Agano la Kale kwenye Biblia. Kwa kweli, urefu wa Agano la Kale unafikia hadi mara nne ya urefu wa Agano Jipya (Agano Jipya likiwa refu zaidi kidogo ya Kurani), hivyo haliwezi kuwako pendekezo kuwa Agano Jipya ni toleo la Agano la Kale lililobadilishwa.



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 8 27-05-2022 14:25:45

## 3. AGANO LA KALE LIMEWAHI KUBADILISHWA?

Kuna ushahidi mwingi hadi leo unaothibitisha kuwa Agano la Kale halijawahi kubadilishwa. Kama ilivyoonyeshwa, Agano la Kale ni andiko la Maandiko Matakatifu ya Wayahudi. Mwislamu aliye tayari kuangalia viashirio vya ukweli huu atatambua mara moja kuwa Agano la Kale kamwe halikuweza kubadilishwa na Wakristo wakiweka Agano Jipya badala yake. Maana Wayahudi hawaamini kabisa kuwa Yesu ndiye Masihi, wala hawaamini kuwa alikufa kwa ajili ya dhambi za wanadamu. Kwa hali hii wanafanana na Waislamu ambao, ingawa wanamtambua Yesu kuwa ni mwanadamu aliyetumwa kutoka kwa Mungu, hawaamini kuwa alikuwa Mwana wa Mungu wala kuwa alikufa kwa ajili ya dhambi zetu. Hili lina maana kuwa kuukataa kwao uungu wa Kristo na kazi yake ya kukomboa hufanana na msimamo wa Wayahudi. Kwa vile Agano la Kale lilivyolindwa na Wayahudi kwa uangalifu tangu kabla ya wakati wa Yesu, haiwezekani kabisa kuamini kuwa Wakristo wangeweza kulibadilisha wakati wo wote katika historia yao.


Tathmini nyofu ya mambo hayo yatatuleta kwenye mahitimisho haya yenye hoja:

1. Agano la Kale lingeweza kubadilishwa tu kama Wayahudi na Wakristo wakati fulani katika historia wangekutana na kukubaliana kulipotosha. Kwa kuzingatia tofauti kati ya Imani hizo mbili uwezekano wa njama kama hiyo siyo tu hauna maana, bali pia hakuna ushahidi po pote katika historia wa kushuhudia upotoshaji kama huo wa Maandiko ya Agano la Kale. Waislamu lazima walifikirie kwa makini jambo hili la hakika kwamba Agano la Kale linatambuliwa na dini mbili tofauti kabisa kuwa ni Neno la Mungu na limedumishwa kwa uangalifu sana na zote mbili bila ya dini hizo kutegemeana. Hivyo haupo uwezekano wa imani moja kati ya hizo kulipotosha andiko, maana kama mmoja angebadilisha, mwingine angekosoa mara moja.



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 9 27-05-2022 14:25:46

2. Ushahidi mwingine wa kuthibitisha kuwa Wakristo hawangeweza kulibadilisha Agano la Kale ni ile tafsiri ya andiko lote kutoka kwenye Kiebrania, lugha yake ya asili, hadi kwenye Kigiriki karne mbili kabla ya wakati wa Yesu Kristo. Tafsiri hii inajulikana kama Septuagint na ilisambazwa kwenye ulimwengu wa Wagiriki wakati wa Ukristo. Hadi leo linakubaliana kabisa na maandiko ya zamani ya Kiebrania cha Kimasoret [Wamasoret walikuwa waandishi wa Kiyahudi walionakili kwa uangalifu maandiko ya zamani ya Kiyahudi yaliyoandikwa kwa mkono] ambayo Wayahudi waliyo nayo na yapo kwenye nyumba za makumbusho na kwenye nyaraka. Maandiko haya yana karibu miaka 1000, na yamehifadhiwa na Wayahudi bila ya kumtegemea Mkristo kwa lo lote.
3. Cha kustusha zaidi ni magombo mengi yaliyopatikana kwenye mapango karibu na Kumran, mashariki mwa Bahari ya chumvi. Kati ya hayo yalikuwa magombo mawili





06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 10 27-05-2022 14:25:46

kamili ya nabii Isaya, yanayokubaliana kabisa na Biblia zetu leo. Magombo haya yaliandikwa miaka 200 kabla ya wakati wa Yesu Kristo. Kwa hiyo siyo tu tuna tafsiri ya Kigiriki inayojitegemea, bali pia tuna maandiko mengi yaliyoandikwa kwa mkono kabla ya enzi ya Kikristo kwa lugha ya asili ya Kiebrania.

***Tunahitimisha:***

Kwa hiyo haiwezekani kuwako pendekezo lenye hoja kuwa Agano la Kale limebadilishwa au kupotoshwa na Wakristo. Zaidi sana haiwezekani kuwa Agano Jipya ni toleo la Agano la Kale lililobadilishwa au ni mbadala wake. Agano Jipya na Agano la Kale ni vitabu tofauti ambavyo vyote vimetunzwa kwa uangalifu na kanisa la Kikristo. Agano la Kale kama tulivyoona, nalo limetunzwa bila uharibufu na Wayahudi kwa wivu mkubwa bila ya kuwategemea Wakristo.

Hivyo je, haitakuwa busara zaidi kuvisoma kwanza vitabu hivi kuliko kushawishiwa na uongo kuhusu yaliyomo na kuleta dhana potovu kuwa Biblia imebadilishwa?

Kwa kuanza tunamhamasisha msomaji akigeukie kiambatisho SAFARI KWENYE BIBLIA ili awe na Mpango wa Kusoma Maandiko (taz. uk.33).



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 11 27-05-2022 14:25:46

## 4. TUJIFUNZE KUTOKA KWENYE HISTORIA

Kwa nini Waislamu wengi leo wanashikilia imani potofu kuwa Wakristo wameibadilisha au kuipotosha Biblia? Tunaweza kuona jambo na mahali maalumu katika historia lilipoanzia dai hili.

Kama uchunguzi ulivyoonyesha, dai kuwa maandiko ya Kikristo yana uongo lilitoka kwa Ibn-Khazem, aliyefia huko Cordoba, Uhispania, mwaka wa 1064.

Akiutetea Uislamu dhidi ya Wakristo, Ibn-Khazem alifikia kuyaamulia kupingana kwa yaliyomo kwenye Kurani na yaliyomo kwenye Injili. Mfano mmoja wa wazi ulikuwa andiko la Kurani "Hawakumwua wala hawakumsulubu" (Sura 4:157). Ibn-Khazem alidai, "Kwa kuwa lazima Kurani iwe ya kweli, ya uongo lazima yawe maandiko ya Injili yanayopinga. Lakini Muhammad anatuambia tuiheshimu Injili. Kwa hiyo, lazima andiko la sasa la Injili limepotoshwa na Wakristo." Msingi wa hoja yake haukuwa kwenye ukweli wa kihistoria, bali kwenye maoni na nia yake mwenyewe ya kuyalinda yaliyomo kwenye Kurani. Hata hivyo, alisababisha Waislamu waukubali uongo ulioleta udanganyifu kuwa mwanzoni kulikuwa na andiko moja tu, yaani Agano la Kale, na kuwa Agano Jipya limekuja badala yake. Mara alikuwa ameingia kwenye njia hii ya kuwaza, hakukuwa chochote kilichoweza kumzuia asilishikilie dai hili. Kwa kweli, ilionekana kuwa ni njia rahisi zaidi ya kuwashambulia wapinzani. "Tukionyesha kuwa vitabu vyao ni vya uongo, watazipoteza hoja wanazoleta kutoka humo." Hatimaye hili lilipelekea atoe kauli ya kubeza kuwa "Wakristo wameipoteza Injili iliyofunuliwa isipokuwa dalili chache alizoziacha Mungu ili ziwe hoja za kuwakabili."

Ili kujibu vizuri hoja hiyo tutafanya vema kuutafakari ukweli kuwa wanazuoni wengi wa Kiislamu wamekubali kuwa andiko la Agano Jipya ni la kweli na la kuaminika. Ushuhuda



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 12 27-05-2022 14:25:46

wao huthibitisha kuwa mahojiano ya Wakristo na Waislamu hayahitaji wakati wote kuzuiwa na dai lililoanzishwa na Ibn-Khazem. Wanahistoria wawili mashuhuri, Al-Mas'udi (aliyekufa mwaka wa 956) na Ibn-Khaldum (aliyekufa mwaka wa 1406), waliutetea uhalisi wa andiko la Injili. Wanatheolojia wanne waliojulikana sana walikuwa na maoni hayo hayo: Ali at-Tabari (aliyekufa mwaka wa 855), Qasim al-Khasani (aliyekufa mwaka wa 860), Amr al-Ghakhiz (aliyekufa mwaka wa 869) na maarufu Al-Ghazzali (aliyekufa mwaka wa 1111). Mtazamo wao wanaushiriki akina Abu Ali Husain Ibn Sina, anayejulikana huko Magharibi kama Avicenna (aliyekufa mwaka wa 1037). Al Bukhari (aliyekufa mwaka wa 870), aliyepata jina maarufu kwa kukusanya mila za kale, aliinukuu Kurani yenyewe (Sura 3:72. 78) ili kuthibitisha kuwa andiko la Biblia halikupotoshwa.[2]

Msomaji akumbushwe kuwa kamwe haijapatikana faida yo yote katika kuuingilia ukweli, maana, kama Kurani inavyoliweka, "Uongofu umekwisha pambanuka na upotofu" (Sura 2:256) au kama Biblia Takatifu inavyotuonya kwa dhati: "Msidanganyike: Mungu hadhihakiwi." (Wagalatia 6:7) Kwenye uchanganuzi wa mwisho wakati wote mdanganyifu atakuwa amejidanganya mwenyewe!

[2] Kutoka CAN WE TRUST THE GOSPEL? na J. Wijngaard



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 13 27-05-2022 14:25:46

## 5. TAURAT NA INJIL KWENYE KURANI

Kuangalia kwa ufupi fundisho la Kurani kuhusu maandiko yaliyoitangulia nako kutasaidia kuiweka wazi asili ya Agano la Kale na Agano Jipya. Kurani huizungumzia Taurat na Injil ("Torati" na "Injili") ya Wayahudi, na ya Wakristo. Kwenye Kurani Taurat huzungumziwa kuwa ni maandiko ya Wayahudi na Injil kuwa ni maandiko ya Wakristo, na maandiko yote yanakubaliwa kuwa yalitoka kwa Mungu (Sura Baqara 2:136 na nyingine). Hivyo Muhammad mwenyewe alitambua kuwa Wayaudi na Wakristo walikuwa na maandiko mawili tofauti, kwa hiyo tusishangae kuiona hali hii kuwa haijabadilika hadi siku ya leo. Kwa hiyo Waislamu wanaoamini kuwa Agano Jipya ni toleo la Agano la Kale lililobadilishwa hawakijui kitabu chao wenyewe cha Kurani (linganisha na Sura Maida 5:69).

Basi, swali linakuwa, Taurat na Injil kwenye Kurani ni sawa na Agano la Kale na Agano Jipya?  Kwa maana ingawa Kurani inaizungumzia Taurat kuwa ni andiko alilopewa Musa na Injili kuwa ni andiko alilopewa Yesu, jambo linalofanya vitabu hivyo kuonekana kama vitabu tofauti na Agano la Kale na Agano Jipya, Kurani pia inavitambua Taurat na Injil kuwa ni vile vitabu ambavyo Wayaudi na Wakristo wenyewe walivitambua kuwa ni maandiko yao matakatifu. Kama Kurani inavyowazungumzia Wayahudi:

> "Na watakuwekaje wewe kuwa hakimu, nao wanayo Taurati yenye hukumu za Mwenyezi Mungu? Kisha baada ya hayo wanakengeuka, na hao si wenye kuamini."
>
> (Surah 5:43)

Kifungu kile kinafundisha wazi kuwa Wayahudi (wametajwa bayana kama wahusika wa kifungu hiki katika aya ya 41) wanayo Torah, kauli inayoweza kuzaa tafsiri moja tu - walikuwa na kitabu hicho wakati wa Muhammad.

Sasa katika historia yao yote, tangu karne nyingi kabla ya kuja Uislamu, Wayahudi wametambua andiko moja tu -



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 14 27-05-2022 14:25:46

vitabu vya Agano la Kale kama tunavyovijua leo. Si chini ya miaka 800 kabla ya Muhammad, Agano la Kale lilitafsiriwa katika lugha ya Kigiriki inayojulikana kama Septuagint. Hivyo Kurani, ikizungumzia Taurat waliyo nayo Wayahudi, inaweza tu kulizungumzia Agano la Kale ambalo inalithibitisha kuwa ni Neno la Mungu lisilobadilishwa. Kadhalika na Injil, yale Maandiko ya Kikristo. Kurani inasema:

> "Watu wa Injil wahukumu kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu ndani yake." (Surah 5:47)

Kwenye Kurani yote "Watu wa Injili" (ahl-ul-Injil) hutambuliwa kuwa ni Wakristo. Kama vile kwa Wayahudi, hapa wanaagizwa kuhukumu mambo kulingana na maandiko waliyofunuliwa. Kwa kuwa onyo hili limetolewa kwa Wakristo wa wakati wa Muhammad, swali la kueleweka linajitokeza, wangewezaje kuhukumu kwa kutumia Injili kama hawakuwa nayo? Kurani inaonyesha wazi kwenye kitabu walichokuwa nacho ambacho Wakristo wenyewe walikitambua kuwa ndiyo maandiko yao matakatifu, na katika historia yote ya kanisa tumetambua na tumekuwa na andiko moja tu - vitabu vya Agano Jipya kama tunavyovijua leo.

***Tunaangalia kwa makini:***

Kurani yenyewe inatambua kuwa Agano la Kale na Agano Jipya ni maandiko yaliyofunuliwa kwa Wayahudi na Wakristo mtawalia. Ni hakika kuwa akitofautisha kwa uangalifu kati ya vile vitabu vitakatifu vya dini hizi kuu mbili, Muhammad ametoa ushahidi wa kukubaliana na tofauti iliyopo kati yake ya vitabu hivyo hadi siku hii ya leo.



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 15 27-05-2022 14:25:46

## 6. KURANI KUHUSIANA NA MAAGANO HAYO MAWILI

Mara kwa mara Waislamu wameniambia kuwa wanalikubali Agano la Kale lakini hawalikubali Agano Jipya. Tumeshaona kuwa Kurani yenyewe inayatambua Maagano yote mawili kuwa ni Neno la Mungu, lakini hapa tutaangalia kwa ufupi ushahidi zaidi ili kuthibitisha kuwa hakuna Mwislamu anayeweza kusema kuwa analikataa Agano Jipya bila ya wakati huo huo kuyakataa mafundisho ya msingi yaliyomo kwenye Kurani.

Mwislamu ameagizwa kuwaamini mitume wote, ni moja ya ibara za msingi za "iman" katika Uislamu. Akiombwa ataje baadhi yake, ataanza na Ibrahimu (Abrahamu), Ishaq (Isaka), Yacoub (Yakobo), Dawoud (Daudi), Suleiman (Sulemani) na Yunus (Yona). Wote hawa ni manabii au mitume wakuu kwenye Agano la Kale ambao kila Mwislamu ameagizwa kumwamini (taz. ukurasa unaofuata).

Kila mmoja ni nabii wa Agano la Kale anayejulikana. Agano la Kale lina historia ya mwanadamu, na hasa historia ya taifa la Kiyahudi, tangu wakati wa Adamu hadi karibu miaka 450 kabla ya wakati wa Yesu Kristo. Manabii hawa huonekana kwenye Agano la Kale mmoja baada ya mwingine kufuatana na orodha tuliyoitoa hapo juu. Hakuna Mwislamu atakayewakataa manabii hawa wa Agano la Kale.

Lakini vipi kuhusu mitume wafuatao ambao nao wametajwa bayana kwenye Kurani, yaani Zakariyya (Zekaria), mwanawe Yahya (Yohana Mbatizaji) na Isa (Yesu)? Na vipi kuhusu Bibi Maryam (Mariamu, mama wa Yesu), mwanamke pekee aliyetajwa kwa jina kwenye Kurani nzima? Mwislamu ye yote angethubutu kutoa rai kwamba hawaamini watu hawa watakatifu?

Sasa watu wote hawa wanne mashuhuri waliishi miaka 400 hivi ya Agano la Kale kukamilika. Hawaonekani kwa majina

## Ulinganishi wa Manabii katika Biblia na Kurani

Ulinganishi wa manabii wa Kurani na wale wa Biblia unaonyesha kwamba wengi wa hawa manabii wanafanana sana kwa majina.

Hata hivyo yafaa izingatiwe kwamba katika Biblia, kanuni za mtu kuitwa nabii ni tofauti sana na zile za Kurani. (Tazama: Kumbukumbu la Torati 18:21-22 na Isaya 41:21-24). Uislamu unafunza kwamba jumla ya manabii wote walikuwa 124,000, lakini Kurani imewataja tu wafuatao kwa majina:

| **Jina katika Kurani** | **Sura** | **Jina katika Biblia** |
|---|---|---|
| Adamu | 2:31 | Adamu |
| Nuhu | 4:163 | Nuhu |
| Ibrahimu | 4:163 | Abramu/Ibrahimu |
| Ishmaili | 4:163 | Ishmaeli |
| Ishaq | 4:163 | Isaka |
| Yaqub | 4:163 | Yakobo |
| Isa | 4:163 | Yesu |
| Ayubu | 4:163 | Ayubu |
| Yunus | 4:163 | Yona |
| Haruni | 4:163 | Haruni |
| Daudi | 4:163 | Daudi |
| Musa | 4:163 | Musa |
| Zakaria | 19:2 | Zekaria |
| Yahya | 19:12 | Yohana |
| Yusufu | 6:85 | Yusufu |
| Eliasi | 6:86 | Eliya |
| Luqmani | 31:12 | - |
| Lutu | 7:80 | Lutu |
| Salih | 7:73 | - |
| Shu'ab | 7:85 | Yethro (?) |
| Uzair | 9:30 | Ezra |
| Dhul Kifl | 21:85 | Ezekieli (?) |
| Ilyasa | 6:86 | Elisha |
| Hud | 7:65 | - |
| Idrisi | 19:56 | Henoko |
| Suleimani | 6:84 | Sulemani |
| Muhammad | 7:158 | - |



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 17 27-05-2022 14:25:46

kwenye kurasa za Agano la kale. Kila mmoja wa hawa wanne, kuhusiana na maisha yao na utambulisho wao kihistoria, ni mtu wa Agano Jipya. Ni kwenye Agano Jipya ambamo Mwislamu atაziona habari za Yohana Mbatizaji na baba yake Zekaria na za Mariamu na Mwanawe Yesu. Hivyo Kurani huwataja mitume na watu watakatifu kutoka kwenye Agano la Kale na pia kwenye Agano Jipya. Kwa hiyo hakuna Mwislamu anayeweza kulikataa Agano Jipya bila ya kuwakataa watu hawa watakatifu wanne ambao Kurani huwahimiza Waislamu kuwaamini. Hivyo tuna ushahidi zaidi kwenye Kurani wa kuukabili uongo wa Waislamu wanaosema hawawezi kulikubali Agano Jipya.

Hata hivyo kama ilivyoonyeshwa mapema, kuna Waislamu wengi wanaoamini kuwa Agano la Kale linafanana na Kurani lakini Agano Jipya ni tofauti na vyote viwili. Dhana potovu inabaki kuwa Agano la Kale lilikuwa andiko la asili na hivyo linakubaliana na Kurani, lakini Agano Jipya ni andiko lililopotoshwa na kwa hiyo linatofautiana na vyote viwili.

Tunamhimiza msomaji aufikirie upya msimamo wake huku akiyatafakari mambo ya hakika yafuatayo:

1. **Namna ya ufunuo** wa Agano la Kale, yaani hii ambayo watu watakatifu wa Mungu waliliandika andiko chini ya uvuvio wa Roho Mtakatifu, katika tabia na namna yake hulingana kama ifuatavyo na:

| | | |
|---|---|---|
| Agano Jipya | : | Inalingana kabisa |
| Kurani | : | Ni tofauti kabisa |

2. Agano la Kale **kusomwa lote** na wafuasi wa hizo dini mbili za Ukristo na Uislamu kuanzia Mwanzo hadi kitabu cha mwisho cha Malaki, ni ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| Na Wakristo | : | Mamilioni ya waumini |
| Na Waislamu | : | Hakuna ye yote |



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 18 27-05-2022 14:25:46

3. Agano la Kale **kutafsiriwa katika lugha nyingine** mara ngapi na Wakristo na Waislamu, ni kama ifuatavyo:

   Na Wakristo : Zaidi ya elfu moja
   Na Waislamu : Hakuna kabisa

4. Agano la Kale **kuambatana na maandiko** ya Wakristo na Waislamu, yaani Agano Jipya na Kurani, na hivyo kuchapishwa kila mwaka kama kitabu kimoja:

   Na Wakristo : Mamilioni ya nakala
   (Agano la Kale na Agano Jipya katika kitabu kimoja)
   Na Waislamu : Hakuna kabisa
   (Agano la Kale na Kurani katika kitabu kimoja)

5. Maandiko ya Agano la Kale **kunukuliwa** mara ngapi kwenye maandiko ya Wakristo na ya Waislamu, ni kama ifuatavyo:

   Kwenye Agano Jipya la Wakristo : Mara 244
   Kwenye Kurani ya Waislamu : Mara moja tu

6. Tunapolisoma Agano la Kale kwa uangalifu ili kuutambua **unabii** unaomtabiri Yesu yule Masihi, na Muhammad, tunaona unabii wao mara ngapi:

   Unamtabiri Yesu : Unabii kama mara 300
   Unaomtabiri Muhammad : Hakuna kabisa

7. Agano la Kale **kusomwa kila wiki** makanisani na misikitini, sambamba na Agano Jipya na Kurani mtawalia, ni kama ifuatavyo:

   Katika makanisa ya Kikristo : Yaliyo mengi
   Katika misikiti ya Waislamu : Hakuna kabisa

8. Nakala za Agano la Kale **kuchapwa na kuchapishwa na kuuzwa** kila mwaka duniani kote, ni kama ifuatavyo:

   Na wachapishaji Wakristo : Mamilioni
   Na wachapishaji wa Kiislamu : Hakuna kabisa



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 19 27-05-2022 14:25:46

***Tunahitimisha na kuuliza:***

Kwa kuuangalia ukweli huu usiopingika haiwezekani kuelewa Waislamu wanavyoweza kuendelea kushikilia uongo kuwa Agano la Kale ni kama ilivyo Kurani na tofauti na Agano Jipya. Au kweli tumekuwa si wakweli wala waaminifu kwenye takwimu na tofauti zilizotolewa hapo juu?

Ukweli hujisemea wenyewe - Agano la Kale na Agano Jipya kwa pamoja ndiyo Biblia ya Kikristo iliyotunzwa, huku Kurani ikisimama peke yake.



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 20 27-05-2022 14:25:46

## 7. SIFA YA KIKRISTO YA AGANO LA KALE

Sababu ya uwekezaji wa Kikristo kwenye Agano la Kale kama ilivyoshuhudiwa kwenye sehemu iliyopita, na kutopenda kwa Waislamu kulisoma wala kulichapisha, inakuwa dhahiri mtu akiiangalia tabia ya Kikristo ya yaliyomo ya Agano la Kale, na hasa unabii kuhusu huyo Masihi. Ingawa ni andiko la Wayahudi, kwa kweli linakubaliana zaidi na ujumbe wa Kristo kuliko dini ya Wayahudi au Uislamu.

Kwanza tunaona kwenye Agano la Kale kuwa Masihi ajaye, ambaye anatambuliwa kuwa ni mpakwa mafuta kwenye Agano Jipya (Yohana 4:25-26) na kwenye Kurani (Surah 3:45), alitabiriwa kuwa ni Mwana wa Mungu ajaye. Kwenye mfano wa zaburi ya Kimasihi tunamwona Mwokozi anayetarajiwa akizungumza kupitia kwa mtangulizi wake, nabii Daudi, kwa maneno yafuatayo:

> *"Nitatangaza amri ya Bwana: Yeye aliniambia, "Wewe ni Mwanangu, leo mimi nimekuzaa."* *(*Zaburi 2:7)

Kwenye matukio mengi katika Agano Jipya maneno haya hutumika kumwonyesha Yesu Kristo (Matendo 13:33; Waebrania 1:5; 5:5). Hivyo tunaona pia Mungu mwenyewe akimzungumzia Masihi ajaye kwa namna ile ile:

> *"Yeye ndiye atakayejenga nyumba kwa ajili yangu, nami nitakifanya imara kiti cha ufalme wake milele. Mimi nitakuwa baba yake, naye atakuwa mwanangu.*
> (1 Mambo ya Nyakati 17:12-13)

Agano la Kale siyo tu linathibitisha kuwa Masihi ajaye, Yesu, atakuwa Mwana wa Mungu, bali pia linaithibitisha sifa nyingine ya maisha yake ambayo Kurani inaikataa (Surah 4:157), yaani kusulubiwa kwake. Mara nyingi Agano la Kale linakutabiri kusulubiwa kwa Kristo, kama kwenye aya zifuatazo:



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 21 27-05-2022 14:25:46

*Wote wanionao hunidhihaki, hunivurumishia matusi, wakitikisa vichwa vyao: Husema, "Anamtegemea Bwana, basi Bwana na amwokoe. Amkomboe basi, kwa maana anapendezwa naye."* (Zaburi 22:7-8)

Maneno haya yalitimia watu waliokuwa wakipita njiani walipomvurumishia matukano huku wakitikisa vichwa vyao na kusema,

*"Wewe ambaye utalivunja Hekalu na kulijenga kwa siku tatu, jiokoe mwenyewe basi! Kama wewe ni Mwana wa Mungu, shuka kutoka msalabani." Vivyo hivyo, viongozi wa makuhani, walimu wa sheria pamoja na wazee wakamdhihaki wakisema, "Aliwaokoa wengine, lakini hawezi kujiokoa mwenyewe! Yeye ni Mfalme wa Israeli! Ashuke sasa kutoka msalabani, nasi tutamwamini. Anamwamini Mungu, basi Mungu na amwokoe sasa kama anamtaka, kwa maana alisema, 'Mimi ni Mwana wa Mungu.' "* (Mathayo 27:40-43)

Zaburi inaendelea ikizungumzia maumivu makali ya Masihi, kama maumivu yale anayoweza kuwa nayo mtu aliyetundikwa msalabani: *Nimemiminwa kama maji, mifupa yangu yote imetoka katika viungo vyake. Moyo wangu umegeuka kuwa nta, umeyeyuka ndani yangu. Nguvu zangu zimekauka kama kigae, ulimi wangu umegandamana na kaakaa la kinywa changu, kwa sababu umenilaza katika mavumbi ya kifo* (Zaburi 22:14-15). Na anaendelea kwenye ushahidi wa wazi kuwa alipigiliwa misumari kwenye msalaba: ... *wametoboa mikono yangu na miguu yangu* (Zaburi 22:16). Tena inaendelea kwa maneno haya: *Wanagawana nguo zangu wao kwa wao, na vazi langu wanalipigia kura* (Zaburi 22:18). Huu ni unabii uliotimia ipasavyo aliposulubiwa Yesu:

*Askari walipokwisha kumsulubisha Yesu, walichukua nguo zake wakazigawa mafungu manne, kila askari fungu lake. Ila walikubaliana wasilichane lile vazi lake kwa maana*



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 22 27-05-2022 14:25:46

*lilikuwa halina mshono bali limefumwa tangu juu hadi chini. Wakaambiana, "Tusilichane ila tulipigie kura ili kuamua ni nani atalichukua." (Yohana 19:23-24)*

Katika zaburi nyingine ya Kimasihi ambayo inaweka vilio vya Mpakwa mafuta wa Mungu akiwa na mateso makali kwenye msalaba, tunakuta maneno yafuatayo, "Waliweka nyongo katika chakula changu na walinipa siki nilipokuwa na kiu." (Zaburi 69:21). Unabii huu vile vile umetimia aliposulubishwa Yesu (Mathayo 27:48; Yohana 19:28-29).

Mahali pengine katika Agano la Kale kuna kifungu kirefu kinachozungumzia kazi ya ukombozi ya Masihi atakayekuja. Kina kauli za wazi za kuonyesha ya kwamba atakufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama ifuatavyo:

*Lakini* ***alitobolewa***
*kwa ajili ya makosa yetu,*
***alichibuliwa*** *kwa maovu yetu,*
*adhabu iliyotuletea sisi amani*
*ilikuwa juu yake,*
*na kwa majeraha*
*yake sisi* ***tumepona****.*

*Sisi sote, kama kondoo,*
*tumepotea,*
*kila mmoja wetu amegeukia*
*njia yake mwenyewe,*
*naye* ***BWANA aliweka juu yake***
***maovu yetu sisi*** *sote.*

*Isaya 53:5-6*



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 23 27-05-2022 14:25:46

Maneno haya yanatumika moja kwa moja kumlenga Yesu katika Agano Jipya (Mathayo 8:17; 1 Petro 2:24). Aya mbili zinazofuata ambazo nazo zinazungumzia mateso yake na kifo chake, nazo zinatumika kwa Yesu katika Matendo 8:35.

Aya inayofuata inasomeka, "Wakamfanyia kaburi pamoja na waovu, pamoja na matajiri katika kifo chake, ingawa hakutenda jeuri, wala hapakuwa na hila kinywani mwake" (Isaya 53:9). Aya hiyo nayo ilitimia kwa Yesu, maana kaburi lake liliandaliwa pamoja na waovu, lakini tajiri Yusufu wa Arimathaya alimwondoa msalabani na kumzika kwenye kaburi lake mwenyewe Yusufu (Marko 15:46). Sehemu ya pili ya aya hii nayo inatumika kuhusu Yesu katika 1 Petro 2:22.

Aya zinazofuata zinazungumzia wazi wazi utayari wake wa kufa kwa ajili ya dhambi za wanadamu na kufufuka kwake:

> *Ingawa BWANA amefanya maisha yakekuwa sadaka ya hatia, ataona uzao wake na kuishi siku nyingi, nayo mapenzi ya BWANA yatafanikiwa mkononi mwake. Baada ya maumivu ya nafsi yake, ataona nuru ya uzima na kuridhika; kwa maarifa yake, mtumishi wangu mwenye haki atawafanya wengi kuwa wenye haki, naye atayachukua maovu yao.* (Isaya 53:10-11)

Hakuna kauli katika Agano Jipya kuhusu kifo cha Yesu msalabani kwa ajili ya dhambi zetu inayokazia zaidi kuliko hii inayotoka kwenye kurasa za Agano la Kale. Sura yote inahitimisha:

> *"Kwa sababu aliyamimina maisha yake hadi mauti, naye alihesabiwa pamoja na wakosaji. Kwa kuwa alichukua dhambi za wengi, na kuwaombea wakosaji". (Isaya 53:12)*

Yesu mwenyewe alitamka kuwa maneno yaliyotangaza kuhesabiwa kwake *pamoja na waovu* yatatimia kwake (Luka 22:37). Mahali pengine kwenye Agano Jipya tunaona tena maneno haya yakinukuliwa kuwa yalitimizwa kwa Yesu akisulubiwa katikati ya wanyang'anyi wawili (Marko 15:28). Maneno ya mwisho: *na kuwaombea wakosaji*, nayo yalitimizwa kwa Yesu alipowaombea msamaha wote waliomsulubisha bila ya



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 24 27-05-2022 14:25:46

makosa: *“Baba, wasamehe, kwa maana hawajui walitendalo!”* (Luka 23:34).

Kwenye vifungu hivi vyote tuna ushahidi mwingi sana kuonyesha kuwa Agano la Kale lina tabia ya Kikristo, na kuwa fundisho lake linapingana na fundisho la Kurani kuhusu Yesu. Ushahidi wote huthibitisha kuwa Agano la Kale na Agano Jipya yana umoja ulio thabiti, huku Kurani ikionekana kutofautiana na Maagano yote mawili kwenye mambo mengi sana.

Miaka kadhaa iliyopita msemaji wa Kikristo alikaribishwa kushiriki na rabi (mwalimu) wa Kiyahudi jukwaani kwenye mjadala wa hadhara katika chuo kikuu cha Witwatersrand huko Afrika Kusini. Mada ilikuwa “Yesu ndiye Masihi?” Akitambua kabisa kuwa umati ule wa Wayahudi hautakubali andiko lo lote lenye uthibitisho nje ya vitabu vya Agano la Kale, msemaji huyo wa Kikristo alinukuu tu unabii wa kuja kwa Masihi unaoonekana kwenye vitabu 39 vya Agano la Kale. Baada ya mjadala mwanafunzi mmoja alimkabili msemaji huyo na kumkosoa akidai amesema uongo, maana vifungu vile viliwasilisha wazi wazi nafsi na kazi ya Yesu Kristo kiasi cha mwanafunzi huyu kushawishika kuwa vifungu vile vimetolewa kwenye Agano Jipya. Ilipoonekana kuwa sivyo, ilibidi akubali na kusema: “Hatujawahi kuvisikia vifungu hivi kwenye sinagogi letu” (mahali pa kuabudia Wayahudi).

Yote haya huelezea kwa nini Wakristo huvichapisha vitabu vya Agano la Kale na Agano Jipya vikiwa pamoja kama kitabu kimoja, Biblia Takatifu, na huvisoma vyote kwa pamoja kwa shauku mwaka mzima. Ndiyo sababu Wakristo huchapisha na kueneza mamilioni ya nakala za Agano la Kale kila mwaka tofauti na Waislamu. Agano la Kale lilitimizwa katika Agano Jipya, si katika Kurani. Vipitie tu vitabu vyote wewe mwenyewe. Msomaji halisi atashawishika hivi karibuni kuwa dhana inayoshikiliwa na wengi kuwa kuwapo kwa Agano Jipya kunaashiria badiliko katika maandiko ya Kikristo haipaswi kuzingatiwa. Kamwe hakuna kiini cho chote kwenye imani kama hiyo.



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 25 27-05-2022 14:25:46

# 8. AGANO LA KALE NA AGANO JIPYA

Hata hivyo bado tuna swali moja. Mtu anaweza kuuliza: Kwa nini vitabu hivi tunaviita Agano la Kale na Agano Jipya? Jibu ni rahisi, vitabu hivi viwili hushughulikia maagano mawili bayana yaliyofanywa na Mungu, moja kupitia kwa Musa na moja kupitia kwa Yesu. La mwanzo linajulikana kama La kwanza linajulikana kati ya Wakristo kama agano la kale, wakati lililofuata ni agano jipya. Uchunguzi kwenye historia ya mwanzo ya Wayahudi utalielezea hili.

Waisraeli walipoondoka Misri wakiongozwa na Musa, Mungu alifanya agano nao kwenye Mlima wa Sinai. Huko aliwapa zile Amri Kumi, zilizowekwa kwenye Agano la Kale katika Kitabu cha Kutoka 20:1-17, pamoja na sheria nyingine nyingi, za kimaadili na za kiibada. Amri hizi ziliweka wajibu kamili juu ya Waisraeli wenyewe kulidumisha agano, wakipewa onyo la wazi kuwa kutotii ko kote juu ya sheria hizi ni kulivunja agano. Musa alisema:

> *"Alaaniwe mtu yule ambaye hatashikilia maneno ya sheria hii kwa kuyatekeleza."* (Kumbukumbu la Torati 27:26)

Zile Amri Kumi na sheria nyingine ziliweka wajibu juu ya Waisraeli kwa kuanzishwa na maneno "Lazima mfanye" au "Msifanye". Kwa kutaja mifano michache tu, Mungu alisema, *"Ni lazima mzitii sheria zangu, na mwe waangalifu kuzifuata"* (Walawi 18:4), *"Kuweni watakatifu"* (Walawi 19:2), *"Ni lazima kuzishika Sabato zangu"* (Walawi 19:3). Na kwa upande wa makatazo, "Usiue, usizini, usiibe, usitoe ushuhuda wa uongo dhidi ya jirani yako" (Kutoka 20:13-16). Kwa kutaja machache tu. (mwenyewe vitabu vyote vya Kutoka na Mambo ya Walawi).

Baada ya amri na sheria zote kuwasilishwa na Musa kwa watu, alilithibitisha agano ambalo Mungu alilifanya nao kwa maneno haya kutoka kwenye Agano la Kale:



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 26 27-05-2022 14:25:46

> *Ndipo Musa akaandika kila kitu* B*WANA* *alichokuwa amesema. Akaamka kesho yake asubuhi na mapema na kujenga madhabahu chini ya mlima na kusimamisha nguzo kumi na mbili za mawe kuwakilisha makabila kumi na mawili ya Israeli. Kisha akawatuma vijana wanaume wa Kiisraeli, nao wakatoa sadaka za kuteketezwa na dhabihu za mafahali wachanga kuwa sadaka za amani kwa* B*WANA*. *Musa akachukua nusu ya damu ya wale wanyama na kuiweka kwenye mabakuli na nusu nyingine akainyunyiza juu ya madhabahu. Kisha akachukua kile Kitabu cha Agano na kuwasomea watu. Nao wakajibu, "Tutafanya kila kitu alichosema* B*WANA*, *nasi tutatii." Ndipo Musa akachukua ile damu, akawanyunyizia wale watu, akasema, "Hii ni damu ya agano ambalo* B*WANA* *amelifanya nanyi kufuatana na maneno haya yote."*
>
> (Kutoka 24:4-8)

Mara baada ya haya kufanyika Mungu alimwita Musa apande mlimani akazipokee mbao mbili za mawe zenye amri kumi (Kutoka 24:12). Lakini Musa aliposhuka kutoka mlimani siku 40 baadaye, alilikuta taifa zima likicheza likiizunguka ndama ya dhahabu waliyoitengeneza Waisraeli. Kwa ibada kama hiyo ya sanamu, tayari kwa tendo hilo moja la uasi wa kutisha dhidi ya Mungu walikuwa wameshazivunja amri na sheria zote alizowapa Mungu. Musa alizivunja zile mbao mbili za mawe kwa kuzitupa chini akitambua kwa uchungu kuwa agano lile lilikuwa limevunjwa kwa makusudi. Mungu akaagiza washiriki wakuu wa jambo lile wauawe, na watu 3000 waliuawa siku ile (Kutoka 32:28).

Kwenye historia yao yote Waisraeli waliendelea kulivunja agano. Waligeukia kuabudu sanamu, walimwacha BWANA, walizivunja amri zake, waliwaua manabii. Wajibu wa kulitunza agano[3], ambao waliahidiwao wenyewe kuwa watautekeleza,

---

[3] Ni muhimu kutambua kuwa agano lilitiwa mhuri kwa damu kumwagika; tutaeleza kwa nini tukija kwenye agano jipya.

ulithibitika kuwa ni mzito mno kwa asili ya mwanadamu kuweza kuutekeleza, kwa vile hali yake inavyouelekea uovu na kutomthamini Mungu kiroho. Taifa lingine lo lote lingeweza kufanya hayo hayo. Agano liligeuka kuwa mzigo. Kama mmoja wa wanafunzi wa Yesu alivyotamka baadaye, likawa agano *"ambalo baba zetu wala sisi hatukuweza kulibeba."* (Matendo 15:10).

Karne nyingi baadaye, taifa la Israeli lilikuwa limeasi sheria za Mungu vibaya sana hata akawaondoa kwenye nchi yao akawapeleka Ashuru, Babeli na nchi nyingine mashariki mwa Israeli. Hata hivyo Mungu kwa huruma alitamka kuwa atafanya agano jipya, na alitamka kupitia mmoja wa manabii wa wakati ule akisema:

> *"Siku zinakuja," asema Bwana, "nitakapofanya agano jipya na nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda. Halitafanana na agano nililofanya na baba zao wakati nilipowashika mkono kuwaongoza watoke Misri, kwa sababu walivunja agano langu, ijapokuwa nilikuwa mume kwao," asema Bwana. "Hili ndilo agano nitakalofanya na nyumba ya Israeli baada ya siku zile," asema Bwana. "Nitaweka sheria yangu katika nia zao, na kuiandika mioyoni mwao. Nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu. Mtu hatamfundisha tena jirani yake, wala mtu kumfundisha ndugu yake akisema, 'Mjue Bwana Mungu,' kwa sababu wote watanijua mimi, tangu aliye mdogo kabisa kwao, hadi aliye mkuu sana," asema Bwana. "Kwa sababu nitasamehe uovu wao, wala sitazikumbuka dhambi zao tena."* (Yeremia 31:31-34)

Bwana Mungu aliahidi kuwa agano hilo jipya halitakuwa kama lile la kale, kwa sababu watu wake hawakuweza kulishika. Badala yake, wakati huu, katika neema na huruma yake, alilichukua mwenyewe jukumu la kulitimiza agano. Mara tano alitoa ahadi akianza kwa maneno *"Nita..."*. Haikuwa hivyo



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 28 27-05-2022 14:25:46

kwenye agano la kale. Hapo alisema *"Mta..., Msi...",* sasa ikawa *"Nita..."*. Mungu alitamka kuwa yeye mwenyewe atahakikisha kuwa agano litakuwa limetimizwa, na alichukua jukumu hilo la kulitimiza. Mwanzoni sheria ziliandikwa kwenye mbao za mawe, sasa zitaandikwa kwenye mioyo ya watu wake, si *kwa wino bali kwa Roho wa Mungu aliye hai, si katika vibao vya mawe, bali katika vibao ambavyo ni mioyo ya wanadamu.* (2 Wakorintho 3:3). Kwa kupitia nabii mwingine wa wakati ule Mungu alifanya ahadi nyingine kuhusiana na hilo agano jipya:

> *Nitawapa moyo mpya na kuweka roho mpya ndani yenu, nitaondoa ndani yenu moyo wenu wa jiwe na kuwapa moyo wa nyama. Nami nitaweka Roho yangu ndani yenu na kuwafanya ninyi mfuate amri zangu na kuwafanya kuwa waangalifu kuzishika sheria zangu.*
>
> (Ezekieli 36:26-27)

Dhamira ilishikiliwa - *"Nita.., Nita.."*. Mungu alijitolea kuhakikisha kuwa watu wake watatunza sheria zake na agano lake. Kisha karne sita zilipita kabla ya agano kufanyika. Usiku wa mwisho ambapo Yesu alikuwa na wanafunzi wake, alikaa nao chakulani na walipokuwa wakila chakula cha jioni alianza kuwaambia kuhusu agano hilo.

> *Kisha akachukua mkate, akashukuru, akaumega, na kuwapa, akisema, "Huu ni mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu. Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu."*
>
> *Vivyo hivyo baada ya kula, akakitwaa kikombe, akisema, "Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu, imwagikayo kwa ajili yenu."* (Luka 22:19-20)

Yesu alipokuwa akiwapa kikombe aliwaambia kuwa ilikuwa ishara ya damu yake itakayomwagika msalabani siku inayofuata, akifa kwa ajili ya dhambi zao; na hasa aliizungumzia damu hiyo kuwa ni damu ya agano jipya. Tumeshaona Musa alivyolifanya agano la kale kwa kuliwekea mhuri kwa damu. Sasa Yesu



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 29 27-05-2022 14:25:46

anasema kuwa kumwagika kwa damu yake mwenyewe kutaliwekea mhuri agano jipya aliloliahidi Mungu mapema kupitia kwa manabii Yeremia na Ezekieli.

Siku kumi baada ya Yesu kupaa mbinguni, Roho Mtakatifu, huyo "Mfariji" maalumu ambaye Yesu aliahidi kuwa atakuja, kweli aliwajia wanafunzi wake (Matendo 2:1-4). Walibadilika kabisa kwa kila namna hata wakawa watu wapya. Walipokea nguvu siyo tu ya kushuhudia kwa furaha kuhusu Masihi (Matendo 1:8), bali pia ya kuzitunza sheria za Mungu, na walijua kuwa dhambi zao zimesamehewa.

Ahadi ya Mungu ilikuwa imetimizwa. Agano la kale lililofanywa na Musa lilikuwa limewekwa kando, na agano jipya, lililofanywa kwa njia ya Yesu, likawapo kwa ajili ya wokovu wa wote wanaomwamini. Lilianzishwa *tumaini lililo bora zaidi ambalo linatuleta karibu na Mungu* (Waebrania 7:19). Kwa kulichukua jukumu yeye mwenyewe, Mungu aliweka agano lililo bora zaidi ili kuwahakikishia wokovu watu wake wote.

> *Lakini huduma aliyopewa Yesu ni bora zaidi kuliko yao, kama vile agano ambalo yeye ni mpatanishi wake lilivyo bora zaidi kuliko lile la zamani, nalo limewekwa misingi wa ahadi zilizo bora zaidi.* (Waebrania 8:6)

Ndiyo sababu sisi Wakristo huyaita maandiko yetu kuwa ni AGANO JIPYA - yanaeleza kwa muhtasari habari za kuwekwa na kutimizwa kwa lile agano jipya. Maandiko ya mwanzo tunayaita Agano la Kale kwa sababu ile ile, yaani yana kumbukumbu za agano la kale. Agano lililofanywa kupitia kwa Musa hatimaye lilifutwa, na agano jipya lililofanywa kwa njia ya Yesu lilianzishwa badala yake. Hili pia litakueleza kwa nini Wakristo hawazishikilii sheria za Sabato (bali huweka kando Jumapili kwa kuabudu na kusifu), au kwa nini hawaleti tena sadaka za wanyama kama alivyoagizwa Haruni, au kwa nini hawaoni tena haja ya kutawadha kiibada kama wakati wa Musa. Haya yote yalikuwa maagizo ya lazima kwa Wayahudi waliokuwa chini



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 30 27-05-2022 14:25:46

ya agano la kale. Lakini kwa kuwa Kristo amelianzisha agano jipya kwa ajili ya watu wake, utakuwa ujinga kurudia desturi za agano la nyuma.

Kwa hiyo unaweza kuona sasa kwa nini tunazungumzia Agano la Kale na Agano Jipya. Hata kuna nakala fulani za Agano Jipya zinazoanza kwa maneno "Agano Jipya, linalojulikana kama Agano Jipya (Kiingereza, testament) la Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo."

***Tunathibitisha:***

Kufuatana na mambo tuliyoyaona sasa, "badiliko" halikuwa kwenye maandiko bali kwenye agano lile lililopo kwenye Agano la Kale. Haijawahi kutokea badiliko au upotoshaji kwenye maandiko ya Agano la Kale, wala Agano Jipya kuwekwa kama mbadala wa Agano la Kale. Lililotokea ni kuwa nafasi ya agano la kale imechukuliwa na agano jipya, mbadala ambao Agano la Kale lenyewe liliutangaza na kuutarajia kwenye vifungu tulivyokuwa tukiangalia kwenye unabii wa Yeremia na Ezekieli.



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 31 27-05-2022 14:25:46

## MASWALI KWA MSOMAJI MAKINI

Sasa tafadhali yapitie kwa uangalifu maswali yafuatayo. Tunatazamia kusikia kutoka kwako na tutazizawadia juhudi zako kwa nakala ya bure ya kimoja cha vijitabu vilivyotajwa nyuma ya chapisho hili.

1. Taja majina ya sehemu mbili kuu za Biblia ya Kikristo.
2. Taja sehemu kuu tatu za Agano la Kale.
3. Tunajua nini kuhusu uhusiano kati ya Kristo na Agano la Kale?
4. Miaka mingapi hutenganisha Agano la Kale na Agano Jipya?
5. Ni kwa misingi gani Ibn-Khazm alidai kuwa Biblia imepotoshwa na Wakristo?
6. Kurani huyaangaliaje maandiko ya Agano la Kale na ya Agano Jipya?
7. Taja majina ya manabii wakuu watano wanaojulikana kwa Wayahudi, Wakristo na Waislamu.
8. Ni sababu gani zinazopendekezwa na mwandishi anapoona kuwa Agano la Kale lina tabia ya “Kikristo”?
9. Ni ipi kauli iliyokaziwa zaidi kuhusu kifo cha Yesu kwenye Agano la Kale?
10. Zile Amri Kumi zinapatikana wapi?
11. Mwenyezi Mungu alitumia mara nyingi maneno gani akitofautisha Agano la Kale na Agano Jipya?



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 32 27-05-2022 14:25:46

## SAFARI KWENYE YA BIBLIA

### *(MPANGO WA KUSOMA MAANDIKO)*

Hongera kwa uamuzi wako wa kujua mwenyewe Biblia inafundisha nini. Kwa hiyo unaanzia wapi kwenye kitabu kikubwa hivyo? Mwanzoni kabisa? Katikati? Uanzie kwenye Agano Jipya au hasa kwenye Agano la Kale? Uanzie po pote?

Wengi wamekuwa wakiuliza maswali haya. Mama mmoja aliielezea hali yake: “Ninakumbuka nilipoikodolea macho Biblia ya kumeremeta niliyokuwa nimepewa hivi punde. Ilikuwa haijawahi kutokea kwangu watu kusoma Biblia mahali po pote ila kanisani (siku za Jumapili pekee). Kwa hiyo ilibidi nianzie wapi? Nikiifungua bila ya utaratibu, nililisoma neno ‘Waraka’. Nilishangaa, Hiyo ni nini? Nilipokuwa nikiusoma ukurasa, niliona neno ‘Mtume’. Hata hili sikujua maana yake. Sikujua pa kuanzia na pa kumalizia, sikuielewa. Huenda kama ninaposoma kitabu kingine cho chote, nianzie mbele!

Lakini nilipokuwa nikiwaza hivyo, rafiki yangu mmoja akaniambia kuwa kinyume na tunavyosoma vitabu vingine vyote, si wazo jema kuanzia mwanzoni mwa Biblia. Alisema, “Biblia ni maktaba ya vitabu vingi, na huwezi kuingia kwenye maktaba ya jumuia ukaanzia kusoma kitabu cha kwanza mlangoni na kuendelea hivi hadi utakapokuwa umezungukia maktaba yote.” [4]

Hapa kuna ushauri wetu uanzie wapi kwenye maktaba hii inayoitwa Biblia:

### WIKI YA KWANZA: Luka 1-24

Fungua ukurasa wa yaliyomo mwanzoni mwa Biblia yako uangalie namba ya ukurasa wa kitabu cha tatu katika sehemu ya Agano Jipya kinachoitwa ‘INJILI KAMA ILIVYOANDIKWA NA LUKA’. Ukisoma sura tatu hadi nne kila siku utazimaliza sura 24 ndani ya wiki moja.

---

[4] Kutoka “How to follow the Shepherd” na Jill Briscoe



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 33 27-05-2022 14:25:46

**WIKI YA PILI: Matendo 1-28**

Sasa geukia kitabu cha tano kwenye AGANO JIPYA chenye jina la 'MATENDO' au 'MATENDO YA MITUME'. Kinaendeleza vizuri ulikotoka maana kiliandikwa na mwandishi yule yule Luka, tabibu, kama kitabu mwenzi. Hizo sura 28 huielezea historia ya mwanzo ya wafuasi wa Yesu ambao baadaye waliitwa 'Wakristo' (Matendo 11:26).

***WIKI YA TATU: Mwanzo 1-11 na Warumi 1-8***

Kwa nini usianzie mwanzo wenyewe wa AGANO LA KALE, kitabu cha MWANZO? Kwa kuwa kina sura 50 huenda kitakuzidi kwa kukisoma ndani ya wiki moja. Lakini hakika utapenda kuimaliza sehemu ya kwanza (Mwanzo ya 1-11) inayoelezea habari za kuumbwa kwa wanadamu na mwenendo wao hadi kwa Ibrahimu, rafiki wa Mungu. Huenda utashtushwa kuona jinsi uasi wa mwanadamu juu ya Muumba wake ulivyouharibu kwa haraka sana uhusiano mzuri wa asili kati ya Mungu na mwanadamu.

Mada hii imeangaliwa tena hatua kwa hatua kwa njia ya utaratibu sana kwenye kitabu cha sita cha AGANO JIPYA kinachoitwa 'WARUMI'. Ukizisoma sura nane za kwanza za waraka wa Paulo kwa Warumi msiba huo wa mwanadamu kumwasi Mungu utaelezewa kwa undani zaidi.

***WIKI YA NNE: Kutoka 1-20***

Sasa rudi kwenye AGANO LA KALE. Usome kitabu cha KUTOKA 1-20 zinazokumbusha kitendo cha Mungu cha ukombozi wenye rehema kupitia nabii Musa, Mungu akiitikia kilio cha Waisraeli waliokuwa utumwani chini ya mamlaka yenye nguvu ya farao wa Misri. Kinaonyesha pia sheria na amri za Mungu kwa watu wake.

Sasa umekuwa safarini kwenye Biblia kwa mwezi mzima na nina uhakika umeipenda. Naomba nipendekeze jambo jipya kwako: Karibu na katikati ya Biblia utaona mkusanyiko wa nyimbo na sala mbalimbali zinazoitwa 'ZABURI'. Mfalme Daudi na wengine walipokuwa wakipitia nyakati tofauti, kama

vile nyakati za mahitaji makubwa lakini pia nyakati za furaha, waliweka mawazo, matumaini, na maombi yao kwa namna ya ushairi. Waumini wengi wa vizazi vyote wameyafanya maombi haya kuwa yao, wakiyatumia mara kwa mara. Kwa nini usisome sura moja au mbili za Zaburi hizo kila jioni kabla hujaenda kulala, ukamwomba Mwenyezi Mungu ajibu na maombi yako?

Mbali na usomaji huu maalumu, yafuatayo ni mapendekezo yetu kwako kwa mwezi wa pili wa safari yako ndani ya Biblia:

### *WIKI YA TANO: Yohana 1-21*

Ukikifungua kitabu cha nne kwenye sehemu ya AGANO JIPYA utaliona jina la 'YOHANA'. Alikuwa mwanafunzi wa karibu sana wa Yesu aliyeyazingatia matukio na mazungumzo na mahubiri mengi muhimu aliyotoa Yesu kwenye umati wa watu, ambayo hayapatikani kwenye habari za Injili nyingine tatu. Ingawa Yohana anatumia idadi ndogo sana ya maneno, ambayo yameteuliwa kwa makini hata idadi yao. Hata hivyo ujumbe wa Yesu, Masihi, unapenya hasa. Soma tu mwenyewe, utaona!

### *WIKI YA SITA: 1 Petro 1-5; 2 Petro 1-3; 1 Yohana 1-5*

Tubaki kwenye AGANO JIPYA na tupitie baadhi ya nyaraka ndogo ndogo kama zilivyoandikwa na Petro na Yohana. 1 PETRO ina sura tano na 2 PETRO sura tatu tu. Utapenda kuongeza na sura tano za 1 YOHANA. Angalia waandishi hao wote wawili wanavyokumbuka waziwazi habari za wakati wakiwa na Yesu, huyo Masihi, alipotembea nao duniani kabla hajapaa mbinguni (ona 2 Petro 1:16-21 na 1 Yohana 1:1-4).

### *WIKI YA SABA: Isaya 40-66*

Sasa turudi kwenye sehemu nyingine ya AGANO LA KALE. Nabii Isaya alishirikisha unabii mzito wa kuja kwa Masihi (soma sura ya 7:14 na 9:6 ili kuchochea hamu yako ya kusoma). Wiki hii jaribu kumaliza sura za 40-66 kwa kusoma kama sura nne kila siku. Zingatia kipekee kauli muhimu kwenye sura ya 53 zilizorudiwa kwenye sehemu nyingine za Biblia.



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 35 27-05-2022 14:25:46

***WIKI YA NANE: Mathayo 1-28***

Tukikamilisha uteuzi wetu wa kiutangulizi wa vifungu kutoka kwenye Biblia Takatifu, zisome sura 28 za kitabu cha kwanza kwenye AGANO JIPYA kinachoitwa ‘‘MATHAYO’. Jina hili linatokana na mwandishi wake, Mathayo, mwingine wa wanafunzi wa Yesu wa karibu waliopata sifa ya kuwa ‘mitume’. Angalia jinsi kitabu hiki kinavyokumbusha misemo maalumu iliyotolewa mamia kadhaa ya miaka ya nyuma kwenye vitabu mbalimbali vya Agano la Kale. Unaweza kupenda kuangalia baadhi ya marejeo zaidi ya 30 ya unabii uliopita, ukauthibitisha mwenyewe ushahidi huu wa kipekee wa unabii wa kimungu.

Tunaamini kuwa wakati huu utakuwa umepata uzoefu na hii “maktaba ya Biblia” na utaweza kuona njia yako mwenyewe ya kuendelea kujisomea Biblia. Wengi wamezoea kusoma sura tatu kila siku na Zaburi moja kila jioni. Mazoea haya yatakusaidia kupitia Biblia nzima ndani ya mwaka mmoja tu.



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 36 27-05-2022 14:25:46

## BIBLIOGRAPHY

Deedat, Ahmed. *Is the Bible the Word of God*. 1980, Durban, Afrika ya Kusini

Fundi, Ngariba Mussa and Ali, Kawemba Mohamed. *Islam in the Bibl*e. 1987, Zanzibar

Gilchrist, John. *What Every Muslim Ought to Know about the Old and the New Testaments,* 1988, Benoni, Afrika ya Kusini

Jadeed, Iskander. *No! The Religion of Christ has not been Abrogated*. The Good Way, Rikon, Switzerland

Muhsin, Ali. *Let the Bible Speak.* Ansaar Muslim Youth Organization, Mombasa, Kenya

Wijngaard, J. *Can we Trust the Gospel?*

### Hitimisho lenye karibisho

Kama kijitabu hiki kimehamasisha fikira yako na ungependa kujifunza zaidi kuhusu maandiko ya Kikristo, tunakukaribisha utuandikie ili tukutumie bure nakala ya kozi zetu AL KITAB. Hii ni kozi yenye masomo 18 kuhusu Biblia na fundisho lake iliyoandaliwa na Wakristo kwa ajili ya Waislamu wanaopenda kuiangalia imani ya Kibiblia kwa mtazamo wa Kikristo.

Pia tuna kijitabu chenye jina la MTU MWENYE UJUMBE kinachokupa taarifa maridhawa kuhusu maneno na mafundisho ya Yesu, yule Masihi. Uamuzi ni wako.



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 37 27-05-2022 14:25:46

**Vijitabu vilivyopendekezwa kwa ajili ya wasomaji wetu:**

1. Umeumbwa kwa Kusudi
2. Jitahidi Kulinganisha
3. Mwisho Usiojulikana
4. Mpendwa Abdallah
5. Mtu Mwenye Ujumbe
6. Kwa nini Kuiamini Biblia
7. Kurani na Biblia
8. Fuata Moyo Wako

Al-Kitab - Kitabu cha Vitabu (kozi ya Biblia kwa njia ya posta)

*Tafadhali nitumie* ..............................................................

.....................................................................................

.....................................................................................

.....................................................................................

Tuma barua yako kwa:

Hamasa ya Milele
S.L.P. 11795
Arusha, TANZANIA
hymilele@gmail.com

Life Challenge
P.O. Box 50770 - 00200
Nairobi, KENYA
info@life-challenge.org



06WhyTrustBible-Swahili-Edited by SB.indd 38 27-05-2022 14:25:46